

**MUHTASARI WA ELIMU YA MKUHUMI KWA WATU WANAOLIMA NDANI AU KARIBU NA MIPAKA YA MSITU WA HIFADHI WA KIJJI**

Kijiji Cha \_\_\_\_\_ Wilaya ya \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_

Jina la anayepewa elimu	Kijiji alichotoka	Wilaya	Simu

Serikali ya Kijiji chetu inakufahamisha kuwa, eneo hili uliloharibu ni Msitu wa Hifahi wa Kijiji, hivyo umetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Kuhifadhi Msitu wa Kijiji zilizoidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji na Halmashauri ya Wilaya. Pia msitu huu upo katika mpango wa MKUHUMI, ambao umelenga kuhifadhi na kulinda Misitu ya Asili yenye umri wa miaka 10 au zaidi. MKUHUMI ni Mpango wa kupunguza uzashaji wa hewa ukaa, inayotokana na ufyekaji na uharibifu wa misitu. Kupitia mpango huu, Kijiji kitapata motisha ya fedha kupitia biashara ya Hewa Ukaa (Karbonidioxide). Kila msitu wenye umri wa miaka 10 au zaidi utakaofyekwa ni hasara kwa Kijiji kwani Motisha ya MKUHUMI itapungua. Hivyo Kijiji kinakuhimiza mtajwa hapo juu kuwa;

- i) Uharibifu uliofanya hapa unapoteza rasilimali muhimu kwa Kijiji kama miti ya mbao, nguzo/fito/majengo, hifadhi vyanzo vya maji na kuboresha hali ya hewa kwenye maeneo yetu,
- ii) Shughuli unazofanya zinasababisha mapato ya MKUHUMI ya Kijiji kupungua. Ili kuepuka Kijiji kupoteza mapato hayo, Kijiji kinakuhimiza kamwe usifyeke mti mwingine wowote wenye umri wa miaka 10 au zaidi ndani ya msitu wa hifadhi wa Kijiji isipokuwa kwa kibali maalum kutoka kwenye kamati ya maliasili ya Kijiji
- iii) Endapo utahitaji kufanya matumizi yoyote ya rasilimali zinazohusiana na msitu wa hifadhi wa kijiji unashauriwa kuwasiliana na uongozi wa serikali ya Kijiji ili kujua kama matumizi hayo yanaruhusiwa au la, kuendana na Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji na Mpango wa usimamizi wa msitu wa hifadhi wa kijiji,

Nakiri kupokea elimu hii naahidi kwamba nitaizingatia		
Jina	Saini	Tarehe

Jina la kiongozi aliyetoa elimu hii			
Jina ya kiongozi	Cheo	Saini	Tarehe